

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI


MKOA WA MBEYA

Simu ya Mdomo: 252957440/252957447

Fax: 025-2590089/2590108

Baruazoteziandikwekwa

MkurugenziMtendaji (W) Mbarali



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P 237,
RUJEWANA.

MAJUKUMU YA KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI

UTANGULIZI

Kitengo cha ukaguzi wa ndani kimeanzishwa chini ya kifungu 45 (1) cha sheria ya fedha ya mamlaka ya Serikali za mitaa Na 13 ya mwaka 1982. Kitengo hiki kinatekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na Kamati ya Ukaguzi.

MAJUKUMU YA KITENGO

- 1) Kuandaa Mpango kazi wa kila mwaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.
- 2) Kufanya ukaguzi kwa Idara na vitengo vyote vya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kama ilivyoainishwa katika mpango kazi.
- 3) Kutoa ushauri kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kuhusu mfumo wa udhibiti wa ndani na ukaguzi wa nje.
- 4) Kuandaa taarifa ya kila robo mwaka na kuiwasilisha kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Mkaguzi wa nje, RAS na Mkaguzi Mkuu wa ndani wa serikali (IAG).
- 5) kutoa ushauri pale utakapohitajika na kufanya ukaguzi maalumu kwa maagizo ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali
- 6) Kukagua na kutoa ushauri sahihi ili kuboresha utawala bora wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.
- 7) Kufanya ufuatiliaji na ukaguzi na usimamizi wa fedha zote za Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali zinakusanywa na halmashauri kwa kutumia mifumo ya kieletroniki.
- 8) Kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha zote za Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali na kuandaa taarifa kwa Afisa Masuuli.

- 9) Kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo na mali za Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali pamoja na kuhakiki uwepo wa thamani ya fedha.
- 10) Kuhakikisha malengo ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali yanafikiwa na kuwa na uwajibikaji.
- 11) Kuhakikisha kuwa sheria, kanuni na taratibu za fedha za serikali zinafuatwa kama zilivyo ainishwa kwenye sheria mbalimbali za serikali
- 12) Kufanya kazi nyinginezo kwa maagizo ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali.

KITENGO KINAFANYA KAZI KWA KUZINGATIA MIONGOZO NA SHERIA MBALIMBALI KAMA IFUATAVYO;

- 1) Public Finance Act no 6 revised 2004 with its regulations.
- 2) Public procurement Act 2004 with its regulations 2005.
- 3) Public scheme of service.
- 4) Public service Act 2002 and its regulation 2003.
- 5) IPPF.
- 6) LAPF 2009.
- 7) Hoja na Maagizo yote ya kisheria.